**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI**

***Ijumaa, 15 Disemba 2023***
***Dar es Salaam.***

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

# MASHIRIKA YA UMMA 16 KUUNGANISHWA NA MANNE KUFUTWA

1. Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 iliielekeza Serikali, pamoja na mambo mengine, "*kuimarisha mashirika ya umma ili yaweze kuendelea kutoa mchango katika maendeleo ya Taifa*" (uk.13). Katika kutekeleza hili, **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,** kupitia hotuba yake ya Bungeni ya tarehe 22 Aprili 2022 alielekeza, pamoja na mambo mengine, "*...kufanya mapitio na uchambuzi wa kina kwenye uendeshaji wa Mashirika ya Umma, tukiwa na lengo la kuyafanya yaweze kujiendesha kwa faida*" (u. 12). Aidha, kupitia falsafa ya 4R, pamoja na hatua zingine, Mheshimiwa Rais alitangaza kufanya mageuzi makubwa katika uendeshaji wa mashirika na taasisi za umma.

2. Katika muktadha ulioelezwa hapo juu, Serikali iliunda Timu ya Wataalam kwa ajili ya kufanya uchambuzi wa kina kuhusu utendaji wa mashirika ya umma kwa lengo la kubainisha changamoto za kiutendaji na kupendekeza hatua za kuchukua katika kuongeza tija ya maendeleo ya nchi.

3. Katika uchambuzi wa utendaji wa mashirika ya umma, Serikali inaongozwa na misingi mikubwa minne. **Mosi,** kuendelea kuongeza ushiriki wa sekta binafsi katika shughuli za uwekezaji na biashara. Katika kutekeleza hili, sekta ya umma itajielekeza katika maeneo yasiyovutia uwekezaji wa sekta binafsi. Mashirika ya umma yatahimizwa kuwekeza katika maeneo ya kimkakati kulingana na majukumu yao. Aidha, Serikali itaelekeza rasilimali nyingi kwenye miradi mikubwa yenye matokeo ya muda mrefu, hususani, ile isiyovutia sekta binafsi kuwekeza.

**Pili,** Serikali kupunguza mzigo wa kuendesha mashirika ya umma yanayohitaji ruzuku ya serikali katika kujiendesha. **Tatu,** Serikali kuendelea kugharamia mashirika ya umma ambayo majukumu yao ya msingi ni kutoa huduma kwa umma na ambayo majukumu hayo kwa asili yake lazima yatolewe na sekta ya umma. **Nne**, mashirika na taasisi zenye mwingiliano na mfanano wa malengo na majukumu yataunganishwa na kuunda shirika au taasisi moja.

4. Kufuatia taarifa na mapendekezo ya Timu ya Wataalam, katika awamu ya kwanza, Serikali imeridhia na kuelekeza kuunganishwa kwa mashirika na taasisi 16 na kufuta mashirika na taasisi za umma nne. Ninatangaza mashirika na taasisi za umma zinazounganishwa na kufutwa kama ifuatavyo:

**A: Mashirika na Taasisi za umma zinazounganishwa:**

(i) Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (*National Identification Authority-NIDA*) na Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (*Registration, Insolvency and Trusteeship Agency -RITA*) yanaunganishwa na kuunda taasisi moja inatayohusika na utambuzi wa matukio muhimu maishani. Lengo ni kutekeleza maelekezo ya Mhe. Rais, ya kuwa na namba moja ya utambulisho (*Single Identification Number*).

(ii) Benki ya Kilimo Tanzania (*Tanzania Agricultural Development Bank -TADB*) na Mfuko wa Pembejeo za Kilimo (*Agricultural Inputs Trust Fund -AGITF*) zinaunganishwa ili kuwa na taasisi moja itakayohusika na mikopo na ugharamiaji wa maendeleo ya kilimo nchini.

(iii) Bodi ya Chai inaunganishwa na Wakala wa Maendeleo ya Wakulima Wadogo wa Chai Tanzania (*Tanzania Smallholders Tea Development Agency -TSHDA*) zinaunganishwa ili kuwa na bodi moja. (Bodi ya Chai).

(iv) Bodi ya Nyama inaunganishwa na Bodi ya Maziwa zinaunganishwa ili kuunda taasisi moja ya kuendeleza na kusimamia mazao ya mifugo yakiwemo ya nyama na maziwa.

(v) Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini (*CARMARTEC*), Taasisi ya Uhandisi na Usanifu Mitambo Tanzania (*TEMDO*) na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (*SIDO*) zinaunganishwa ili kuunda taasisi moja.

(vi) Kituo cha Uwekezaji Tanzania (*TIC*) kinaunganishwa na Mamlaka ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje (*EPZA*) ili kuunda taasisi moja itakayoratibu uwekezaji wa sekta binafsi wa ndani na kutoka nje ya nchi.

(vii) Taasisi ya Utafiti wa Chai Tanzania (*Tea Research Institute of Tanzania - TRIT*), Taasisi ya Utafiti wa Tumbaku Tanzania (*Tobacco Research Instititute of Tanzania -TORITA*) na Taasisi ya Utafiti wa Kahawa (Coffee Research Institute of Tanzania – (TACRI) zinaunganishwa na kuwa sehemu ya muundo wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (*TARI*).

**B: Mashirika na Taasisi za Umma zinazofutwa/kuvunjwa;**

(i) Shirika la Uzalishaji la Jeshi la Polisi ***(Tanzania Police Force Corporation Sole -TPFCS)*** linafutwa.

(ii) Taasisi ya Chakula na Lishe ***(Tanzania Food and Nutrition Centre – TFNC)*** inafutwa.

(iii) Shirika la Elimu Kibaha **(*Kibaha Education Center - KEC*)** linavunjwa na kuunda Shule ya Sekondari Kibaha ama kwa jina ambalo Mamlaka husika zitaamua na Chuo Cha Ufundi. Kwa uamuzi huu hospitali ya Tumbi Kibaha haitakuwa tena sehemu ya Shirika la Elimu Kibaha bali hospitali ya Mkoa wa Pwani. Msajili wa Hazina ameshaelekezwa kukamilisha taratibu husika za makabidhiano na Wizara ya Afya.

(iv) Bodi ya Pareto inafutwa na shughuli zake zitahamishiwa katika Mamlaka ya Usimamizi wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (***CEREAL AND OTHER PRODUCE REGULATORY AUTHORITY-COPRA)***.

**5. Katika mchakato huu, mambo matatu yafuatayo yatazingatiwa:**

(i) Hakuna mtumishi atakayepoteza ajira yake. Maslahi yote watumishi ya umma katika mashirika na taasisi husika yatalindwa na kuzingatiwa kikamilifu kwa kuzingatia sheria na kanuni za utumishi wa umma. Izingatiwe kuwa katika mashirika na taasisi nyingi za umma na serikali kwa ujumla kuna upungufu mkubwa wa watumishi wa umma. Kwa hivyo, watumishi wote ambao mashirika na taasisi zao zinaguswa na zoezi hili watapangiwa kazi zingine katika utumishi wa umma na maslahi yao yatazingatiwa ipasavyo.

(ii) Mchakato wa kufuta na/au kuunganisha mashirika na taasisi za umma utazingatia sheria ambazo zimeanzisha taasisi hizo. Ni kwa sababu hii, uamuzi ninaoutangaza hapa tayari ulishawasilishwa kwa Mawaziri husika ambao ndio wenye nyezo husika ***(Ministerial Instrument Holder)*** kwa hatua zao stahiki.

(iii) Mawaziri husika wameshaelekezwa kuhakikisha kuwa mchakato wa kufuta na/au kuunganisha mashirika na taasisi za umma zilizotangazwa uwe umekamilika ndani ya mwaka huu wa fedha.

(iv) Mageuzi katika utendaji na uendeshaji wa Mashirika ya Umma ni zoezi endelevu. Serikali itaendelea kuimarisha mifumo ya kupima na kutathimini utendaji wa mashirika na taasisi za umma kwa lengo la kuongeza tija katika maendeleo ya nchi.

**Imetolewa na;**

Mhe. Prof. Kitila Alexander Mkumbo **(Mb.)**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI.**

Kwa mawasiliano na taarifa zaidi:

**Immaculate Makilika**

**Simu: 0717 029026**

**Email: immaculata.makilika@planninginvestment.go.tz**